JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

MTWARA FEBRUARI, 2023

TAKUKURU MTWARA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SH. BILIONI 14

Katika kipindi cha Oktoba – Desemba 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mtwara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, huku mkazo ukiwekwa katika UZUIAJI RUSHWA pamoja na elimu ya kuhamasisha wananchi washiriki kikamilifu hasa katika eneo la uwajibikaji na kuchukua hatua stahiki ili kuzuia rushwa, kwakuwa jukumu la kuzuia rushwa ni la kila mmoja wetu kwa nafasi yake.

1. 0 UZUIAJI RUSHWA:

Katika eneo la **UZUIAJI RUSHWA**, TAKUKURU Mkoa wa Mtwara **imefuatilia utekelezaji wa miradi thelathini na saba (37)** yenye thamani ya zaidi ya **shilingi bilioni 14** (14,775,877,702.5/=) katika sekta za Ujenzi, Elimu, Afya, Maji pamoja na ujenzi wa madarasa.

Miradi 10 (sawa na asilimia 27), yenye thamani ya Sh. 7,303,822,067/= ilikuwa na maupungufu na hatua kadhaa zilichukuliwa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini ili kukabiliana na mapungufu hayo;

Na.	JINA LA MRADI NA THAMANI	KILICHOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1	Ujenzi wa shule ya sekondari Namtumbuka. shs. 470,000,000/=	Nyufa katika msingi na baadhi ya kuta za jengo.	Msimamizi wa mradi (Mhandisi wa Wilaya) aliagizwa kurekebisha hilo.

2.	Mradi wa uchimbaji wa kisima cha maji – Hosipitali ya Rufaa Ligula. shs. 13,249,040/=	i. Ufungaji wa vifaa ambavyo vipo tofauti na mkataba - Specifications ii. Mradi kutofanya kazi kama ilivyotarajiwa.	Uchunguzi ulifanyika na kukamilika na kwa sasa jalada lipo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi.
3.	Ujenzi wa kichomea taka Hosipitali ya rufaa ya mkoa – Ligula. shs. 96,184,160/=	i. Utumiaji wa vifaa visivyo na ubora. ii. Kutokamilika kwa mradi kwa wakati na kufanya kazi isiyo na ubora.	Uchunguzi ulifanyika na kukamilika na makubaliano yalifanyika kati yetu na Mkandarasi ili akamilishe kazi.
4.	Bwalo la chakula – Hosipitali ya Rufaa ya Ligula. shs. 61,493,000/=	Kutokamilika kwa mradi pamoja na kulipwa fedha ya kazi zote.	Uchunguzi ulifanyika na kukamilishwa na makubaliano baina yetu TAKUKURU (M) na Mkandarasi ni kwamba akamilishe kazi hizo.
5	Mradi wa matengenezo (upgrading) ya barabara ya Nanyamba - Mbembaleo - Kitaya kwa kiwango cha lami (bitumen) Km 1 na kiwango cha Double surface Dressing kwa Km 1. shs. 974,987,585/=	Kutokuwepo kwa bango la Mradi.	Wakandarasi waliagizwa kuweka mabango ya miradi yao husika.
6.	Mradi wa matengenezo (upgrading) ya barabara ya Nanyamba – Nitekela –Nyundo (km 1.035). shs. 849,849,900/=	Kukosekana kwa ubora wa ufundi katika baadhi ya kazi (poor workmanship)	Mkandarasi aliagizwa kurekebisha mapungufu hayo.

7.	Mradi wa maji Mitambo-Msimbati. shs. 1,809,058,382/=	i. Hakuna Ofisi ya Site na ya kutunzia vifaa vya Mkandarasi. ii. Hakuna vipimo vilivyofanyika kwa ajili ya vifaa kama mchanga, kokoto, maji, nk kama vinakidhi matumizi ya ujenzi. iii. Kutokamilika kwa mradi.	TAKUKURU (M) iliagiza malipo yasifanyike kwa kazi ya ujenzi wa Ofisi ya site pamoja na ya kutunzia vifaa. Pia, anatakiwa kufanya vipimo vya vifaa anavyotumia. (Material test). Kushauri kuwa Mshitiri asitishe Mkataba na Mkandarasi huyo kwa kutokamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba.
8.	Ujenzi wa nyumba ya watumishi (three in one) katika kituo cha Afya Kata ya Mkunwa. shs. 110,000,000/=	Mawe yaliyoletwa eneo la ujenzi kukosa ubora kwa matumizi.	Msimamizi wa mradi aliagizwa kuhakikisha mzabuni wa mawe anayarejesha mawe hayo kwani hayafai kabisa katika ujenzi wa jengo imara.
9	Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Mtwara. Tshs. 2,699,000,000/=	Sehemu ya baadhi ya kuta kuonekana na ufa.	Msimamizi pamoja na Mkandarasi waliagizwa kurekebisha mapungufu hayo.
10.	Mradi wa ujenzi wa Nyumba mbili za wakuu wa idara katika Halmashauri ya Mji Nanyamba. Tshs. 220,000,000/=	Paa la majengo hayo kuonekana kuvuja kipindi mvua ikinyesha.	Msimamizi aliagizwa kuhakikisha mapungufu hayo yanatatuliwa.

1.1 UCHAMBUZI WA MIFUMO:

Pale ambapo eneo la utendaji au utoaji huduma linaonekana au kulalamikiwa kuwa na viashiria vya rushwa, TAKUKURU hufanya **uchambuzi wa mfumo** ili kubaini iwapo kuna mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuiziba. Hivyo katika kipindi husika:-

Tumefanya **chambuzi tatu** za mifumo katika sekta ya biashara, fedha na ujenzi. Chambuzi hizi na Malengo ya chambuzi ni kama yalivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:-

Na.	MFUMO	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1.	**Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko ya biashara,**	• Kutokuwepo kwa kumbukumbu za makusanyo ya ushuru katika soko. • Kukosekana kwa mfumo ulio wazi wa ugawaji wa maeneo katika masoko hayo kwa ajili ya biashara. • Masoko mengi hayana kitabu cha kumbukumbu kinachoonesha idadi ya wafanya biashara waliopo katika masoko husika. • Uwiano usio sawa wa mapato ukilinganisha na idadi ya wafanya biashara wanaoendelea na biashara kwenye masoko. • Wafanyabiashara kutolipa ada na tozo kwa wakati.	Maandalizi ya kufanya warsha na wadau kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo ili kuweka maazimio ambayo yataboresha mfumo na kutokomeza mianya yote ya rushwa.

2.	**Ununuzi kutumia Force Account (Kikosi Kazi) katika Halmashauri**	• Uchaguzi wa wazabuni kwa kuwashindanisha na wasio na sifa au wazabuni hewa. • Uchaguzi wa mafundi (local fundi) bila kufuata taratibu za ushindani. • Kamati za usimamizi kutotekeleza majukumu yao licha ya kuteuliwa na hivyo kudhoofisha usimamiaji wa wananchi. • Utunzaji hafifu wa kumbukumbu za vifaa vilivyonunuliwa, vlivyopokelewa na vilivyotumika.	Maandalizi ya kufanya warsha na wadau kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo ili kuweka maazimio ambayo yataboresha mfumo na kutokomeza mianya yote ya rushwa.
3.	**Ukusanyaji wa mapato na ushuru katika vijiji:**	• Ushuru na mapato yanayokusanywa kutowasilishwa kwa wakati benki. • Ukosefu wa kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato na matumizi yake katika kijiji.	Maandalizi ya kufanya warsha na wadau kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo ili kuweka maazimio ambayo yataboresha mfumo na kutokomeza mianya yote ya rushwa.

2. UELIMISHAJI UMMA:

Kazi za Uelimishaji Umma zilizofanyika ni zifuatazo:-

NA	KAZI	UFAFANUZI
1	Kutembelea na kuimarisha klabu za wapinga Rushwa katika shule za msingi na Sekondari na vyuo	klabu za wapinga Rushwa 88 zilizopo katika shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo ziliimarishwa kwa kupewa elimu ya kukuza uzalendo na uadilifu.

2	Uelimishaji kwa njia ya vyombo vya habari.	Vipindi vya redio 9 vilirushwa kuelimisha wananchi juu ya nafasi yao katika kuzuia rushwa na hasa katika miradi ya maendeleo.
3	Mikutano ya hadhara vijijini ili kuwafikia wananchi wengi walioko pembezoni.	Ilifanyika mikutano ya hadhara 21 ambapo wananchi walihimizwa kushiriki na kusimamia miradi ya maendeleo ili kuzuia rushwa na kuhudhuria mikutano ya vijiji ili kutoa michango yao na kuhoji mapato na matumizi ya kijiji pale ambapo wanaona kuna shida.
4	Semina watumishi wa umma makazini na kutoa elimu juu ya rushwa mahala pa kazi.	Semina 27 zilitolewa kwa lengo la kuwakumbusha watumishi kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo na kujiepusha na vitendo vya Rushwa.
5	Utoaji wa habari na mkala.	Makala 6 na taarifa kwa umma 1 zilitolewa ili kufahamisha umma juu ya mambo yanayofanyika katika uzuiaji rushwa pamoja na kuhabarisha umma juu ya utendaji wa TAKUKURU (M) Mtwara.

Vilevile elimu ya rushwa ilitolewa kwa wateja wanaotembelea ofisi zetu na kutaka ushauri na kugawiwa machapisho mbalimbali kwa ajili ya rejea.

2.1 SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINADAMU KITAIFA

Katika Siku Ya Maadili Na Haki Za Binadamu Kitaifa yaani Desemba 10, 2022, Watumishi wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara waliwatembelea na kuwafariji watoto **233** wanaoishi kwenye mazingira magumu ambapo ujumbe wa Maadili wenye kauli mbiu "*Maadili, Haki za Binadamu, Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa ni Jukumu la Pamoja kati ya Serikali, Wananchi na Wadau wengine*" ulitolewa kwa viongozi wa kanisa la Morovian, walezi, walimu na watoto hao katika kituo cha kanisa la Moravian kilichopo Mbae - Kata ya Ufukoni wanapokusanyika kila Jumamosi.

Aidha watoto hao walifarijiwa kwa kupatiwa mchele, mafuta ya kupikia, sukari na sabuni.

Kwa TAKUKURU wilaya ya Newala watumishi waliwatembelea wanafunzi wa sekondari ya Nangwanda na Newala wanoishi kwenye mazingira magumu na kuwafariji kwa kuwapatia shajala, mashuka na taulo za kike na kutoa ujumbe wa maadili.

Watumishi wa TAKUKURU wilaya ya Tandahimba waliadhimisha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kwa kutembelea hosipitali ya wilaya ya Tandahimba na kuwafariji wagonjwa kwa kugawa sabuni, maji ya kunywa na sharubati.

3. **UCHUNGUZI NA MASHTAKA:**

Pamoja na kuhamasisha sana suala la **KUZUIA RUSHWA,** bado wapo ambao hufanya TAKUKURU ilazimike kufanya kazi za mapambano dhidi ya Rushwa.

Katika kipindi husika, tumepokea **malalamiko 81,** ambapo **taarifa za rushwa zilikuwa 58** na **zisizo za rushwa ni 23.**

- Taarifa 58 zinazohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo: Utawala (21); Ushirika (8); Ardhi(4); Ujenzi(4); Afya (4); Elimu (2); Biashara (2); Ajira(2); Mahakama(2); Nishati(2); TASAF (1); Siasa (1) na Sekta binafsi (5).

- Taarifa 58 zinazohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwa kuanzisha uchunguzi.

- Kupitia uchunguzi huo, Majalada **7** yamekamilika na hakuna mashauri mapya yaliyofunguliwa mahakamani katika kipindi tajwa na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani kusalia **12.**

- Idadi ya mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hiki ni **matatu** ambapo Jamhuri ilishinda katika mashauri **mawili.**

- Taarifa **23** zisizohusu rushwa, wahusika walishauriwa mahali sahihi pa kuziwasilisha na wengine walieleweshwa na kuridhika hivyo taarifa hizo zikafungwa.

Katika hatua nyingine: kwa upande wa kesi zilizotolewa maamuzi Mshitakiwa katika **kesi Na. ECC 03/2022** iliyotolewa hukumu Tarehe 9/11/2022 na mshitakiwa kukutwa na hatia baada ya kufanya maridhiano ya kukiri kosa (Plea bargaining) na hivyo kutakiwa kulipa faini ya shilingi 20,000/= na fidia ya kiasi cha shilingi 4,431,000/= .

Aidha katika kesi nyingine Na. **CC 56/2022** iliyotolewa hukumu Tarehe 30/11/2022 na mshitakiwa kukutwa na hatia baada ya kufanya maridhiano ya kukiri kosa (Plea bargaining) na hivyo kutakiwa kulipa faini ya shilingi 500,000/= na fidia ya kiasi cha shilingi 2,000,000/=.

4. MIKAKATI YA JANUARI– MACHI 2023:

TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, inatarajia katika robo ya Januari-Machi, 2023, kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa kwa kukagua miradi ya maendeleo na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika vita dhidi ya rushwa kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo vipindi vya redio pamoja na uelimishaji katika mikusanyiko mbalimbali.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na matumizi ya fedha za umma na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma. Aidha, tutafanya warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya kuziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

Pia tumejipanga kupitia programu ya TAKUKURU- Rafiki, kushirikiana na wananchi na wadau katika kutambua na kutatua kero katika utoaji wa huduma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo amabazo zikiachwa pasipo kutatuliwa au kupatiwa ufumbuzi zinaweza kusababisha kutokea

kwa vitendo vya rushwa kwenye jamii husika. TAKUKURU- Rafiki ni progaramu ambayo TAKUKURU imedhamiria kuongeza wigo wa ushiriki wa wananchi na wadau katika mapambano dhidi ya Rushwa nchini. Kauli mbiu inayoiongoza progamu hii ni " **Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu; Tutimize Wajibu Wetu**"

5. **HITIMISHO:**

Mwisho, tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa kutuunga mkono katika vita hii yetu sote. Tunawasihi wengine wote wenye mtazamo kwamba hii ni kazi ya Serikali pekee waachane na fikra hizo na wajiunge nasi ili kuongeza nguvu katika jeshi la wazalendo, waadilifu na wanaojisikia fahari kuzuia rushwa. **Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu; Tutimize Wajibu Wetu.**

Imetolewa

JUMBE M. MAKOBA
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) MTWARA
0738150156